



Kumb.Na. TMC/M/56/48

Tarehe: 17/02/2022

## **TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA WAANDIKA NAMBA ZA NYUMBA KWA AJILI YA ANWANI ZA MAKAZI NA POSTI KODI**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Tabora anapenda kuwatangazia nafasi za ajira ya muda kwa nafasi ya uandikaji wa namba za nyumba kwa ajili ya anwani za makazi na posti kodi katika kata nafasi 175, Kutengeneza na kusimika vibao vya majina ya barabara nafasi 175 na, Wakusanya taarifa za mfumo wa anwani za makazi nafasi 175 kwa vijiji na mitaa yote ya Manispaa ya Tabora.

Tarehe ya mwisho wa kupokea maombi ni 25-02-2022 saa 9.30 alasiri.

Tarehe ya kufanya usaili kwa waandikaji wa namba za nyumba ni 26-02-2022.

Tarehe ya kufanya usaili kwa watakaotengeneza na kusimika vibao vya majina ya barabara ni tarehe 04-03-2022.

Tarehe ya kufanya usaili kwa Wakusanya taarifa za mfumo wa anwani za makazi ni tarehe 15-03-2022.

### **A. SIFA ZA MWOMBAJI**

- Awe Raia wa Tanzania mwenye umri kati ya miaka 18-35.
- Awe na Elimu kuanzia kidato cha Nne na kuendelea.
- Awe na uwezo wa kusoma ramani za mitaa.
- Awe na mwandiko mzuri na kasi kubwa ya uandishi.
- Aweze kufika eneo la kazi kwa wakati.
- Awe ni mkazi wa Kata husika.

### **B. KAZI NA MAJUKUMU**

- Kuandika namba za anwani za makazi kwenye mlango wa nyumba, jengo, ukuta na geti.
- Kuwasilisha kwa Mkurugenzi idadi ya nyumba alizoandika kila siku
- Kuhakikisha kuwa namba za nyumba zinaonekana na kusomeka vizuri

### **C. MAOMBI YAAMBATANISHWE NA**


- Nakala ya cheti cha kidato cha nne na kuendelea
- Nakala ya cheti cha kuzaliwa
- Picha (Passport size – 2)
- Barua ya maombi ipite kwa Mtendaji wa Mtaa na Kata unapoishi

### **D. JINSI YA KUTUMA MAOMBI**

Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono zikiwa na anwani kamili ya mwombaji, namba ya simu na barua pepe.

Barua zote ziwasilishwe Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Tabora kwa anwani ifuatayo:

**MKURUGENZI WA HALMASHAURI  
MANISPAA YA TABORA  
S.L.P 174  
TABORA**

  
Dr. Peter M. Nyanja  
**MKURUGENZI WA MANISPAA  
TABORA**

**MKURUGENZI WA HALMASHAURI  
S. L. P. 174  
TABORA**